Amri 10 za Mungiu
1-Usiwe na miungu mingine ila mimi 2-Usijifanyie sanamu ya kuchonga. 3-Usilitaje bure jina la BWANA Mungu wako. 4-Ikumbuke siku ya sabato uitakase 5-Waheshimu baba yako na mama yako. 6-Usiue 7-Usizini 8-Usiibe 9-Usitoe ushuhuda wa uongo dhidi ya jirani yako. 10-Usiitamani nyumba ya jirani yako. Utakutana naye Mungu uso kwa uso siku ya Hukumu. Anachukulia tamaa kama kuzini, "Ye yote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake. "Mathayo 5:28) Anatazama chuki kama mauaji, "Ye yote amchukuae ndugu yake au dada yake ni mwuaji ndani yake. "(Yohana 1. 3:15) Je, utaona ufalme wa Mbinguni? Hili ni jaribio la haraka. Je, Umewahi kusema uongo, kuiba kitu chochote, kulitaja bure jina la Mungu au kuangalia kwa kutamani? Yakobo 2:10 inasema"Kwa maana mtu ye yote anayeishika sheria yote lakini akajikwaa katika kipenglel kimoja tu, ana hatia ya kuivunja sheria yote." Utakuwa na hatia siku ya hukumu? Kama umefanya vitu hivyo Mungu anakutazama kama anaedanganya, anayeiba, analitaja jina la Mungu bure, anayezini kwa roho. Bibilia inaonya kwamba kama unahatia utaenda jehanamu. Mungu alimtuma mwanawe kuteseka na akafa msalabani. Yesu alikubali kuadhibiwa, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu anwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. "(Yohana 3:16) Hatimaye Yesu alifufuka kutoka kwa wafu na akashinda kifo. Tubu (jitenge na dhambi) leo na umwamini yesu, na Mungu atakupa uzima wa milele. Soma bibilia na utii yote ambayo unasoma.

Neno la Mungu I
Yesu akamjibu, "Amin amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Munugu asipozaliwa mara ya pili". (Yohana 3:3) Sisi sote, kama kondoo, tumepotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe (Isaya 53:6) Mimi BWANA huchunguza moyo na kuzijaribu nia kumlipa mtu kwa kadiri ya matendo yake yanavyostahili. (Yeremia 17:10) Nyinyi nanyi msipotubu, mtaangamia vivyo hivyo. (Luka 13: 3) Alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema zake. Alituokoa kwa ktuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu.(Tito 3:5) Iko njia ionekanayo sawa kwa mtu, bali hema la mnyofu litastawi. (Mithali 14:12) Yesu akawaambia, "mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu". (Yohana 14:6) Kwa hiyo hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria, kwa maana sheria hutufanya tuitambue dhambi. (Warumi 3:20) Yeye mwenyewe alizichukuwa dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa. (1 Petero 2:24)Kkwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yasemayo maandiko, ya kuwa alizikwa na alifufuka siku ya tatu. (1Wakorintho 15:3-4) Kwa maana mmeokolewakwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, Si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.(Waefeso 2:8-9)

NENO LA MUNGU II
Amini Neno la Bwana na utaokolewa. Yesu akawajibu, "Kazi ya Mungu ndiyo hii: Mwaminini Yeye aliyetumwa Naye."(Yohana 6:29) Amin amin ninawaambia, yeyote anayesikia maneno yangu na kumwamini yeye aliyenituma, anaouzima wa milele, naye hatahukumiwa, mbali amepita kutoka mautini na kuingia uzimani. (Yohana 5:24) Aliye naye mwana wa mungu anaouzima, yeye asiye na mwana wa Mungu hana uzima. (1 Yohana 5:12-13) Kubali Yesu mbele za watu. Kama mtu yeyote akinionea aibu mimi na maneno yangu, mwana wa adamu atamuonea aibu mimi na maneno yangu mwana wa adamu atamuonea aibu mtu huyo atakapo kuja katika utukufu wake na katika utukufu wa baba na wa malaika watakatifu. (Luka 9:26) Kwa sababu kama ukikiri kwa kinywa chako kwamba "yesu ni bwana" na kwaamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini na hivyo kuhesabiwa haki. Tena kwa kinywa mtu hukiri na hivyo

kupata wokovu. (Warumi 10: 9-10) Ndugu zangu yafaa nini ikiwa mtu atadai kuwa anayo imani lakini hana matendo? Je, imani kama hiyo yaweza kumuokoa? (Yakobo 2:14) Kwa maana Mungu ndiye atandaye kazi ndani yenyu kutaka kwenye na kutenda kwenyu kwa kulitimiza kusudi lake njema. (Wafilipi 2:13) Hivyo basi kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe kwa Mungu. (Warumi 14:12) Lakini msipoona vyema kumtumikia BWANA chagueni hivi leo mtakaye mtumikia lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia bwana. (Yoshua 24:15)

Mpango Rahisi wa Wokovu wa Mungu I
Kwa hiyo usishangaye ninapokuambia hunabudi kuzaliwa mara ya pili. (Yohana 3:7) Katika Bibilia, Mungu anatupa mwelekeo jinsi ya kuzaliwa mara ya pili. Kwanza, lazima ugunduwe kuwa wewe ni mwenye dhambi. "Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. (Warumi 3:23) Kwa sababu wewe ni mwenye dhambi, umehukumiwa kifo. "kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. (Warumi 6:23) Hii inao utenganisho wa milele kutoka kwa Mungu, katika Jehanamu. "Kama vile mwanadamu alivyowekewa kufa mara moja tu na baada ya kufa akabili hukumu. (Waibrania 9:27) Kwa maana Muungu aliupenda ulimwengu akamtoa mwanawe wa pekee, Yesu, ili abebe dhambi zako na afe kwa niaba yako. "Lakini Mungu anaudhihirisha upendo wake kwetu kwamba tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwaajili yetu. Warumi 5:8)
Ijapokuwa hatuwezi kuelewa vipi, Mungu alisema kwamba dhambi zetu ziliwekelewa kwake Yesu na akafa kwa niaba yetu. "Zamani wakati wa ujinga, Mungu alijifanya kama haoni, lakini sasa anawaamuru watu wote kila mahali watubu". (Matendo 17:30) Kutubu kunamaanisha kujitenga na dhambi na kukubaliana na Mungu kwamba mtu ni mwenye dhambi, na hata pia kukubaliana na kile ambacho Yesu alifanya msalabani. "Kisha akawaleta nje akisema "bwana zangu, nifanye nini ili nipate kuokoa?" (Yohana 1:12) Jibu: Mwamini Yesu aliyezibeba dhambi zako, akafa kwa niabaa yako, akazikwa na ambaye Mungu alimfufua. Kufufuka kwake kunatuhimiza kwamba tunaweza kudai uzima wa milele wakati ambapo Yesu alitupokea sisi kama Mwokozi. "Bali wote waliyompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale waliaminiyo jina lake". (Yohana 1:12)

Mpango Rahisi wa Wokovu wa Mungu II
Kwa maana "kila mtu atakayeliita jina la bwana ataokoa". (Warumi 10:13) Amini, Na utaokolewa. Hakuna Kanisa au kazi nzuri ambayo inaweza kukuokoa. Kumbuka, Mungu ndiye anayefanya ukombozi. Mpango rahisi wa wokovu wa Mungu ni: Wewe ni mwenye dhambi na isipokuwa uokoke na umwamini Yesu aliyekufa kwa niaba yako, utatumikia maisha yako yote katika jehanamu. Kama utamwamini kama aliyesurubiwa, akazikwa, na akafufuka Mwokozi, utasamehewa dhambi zako zote na zawadi ya wokovu wa milele kwa imani. Kama mpango wake haueleweki vyema, soma hii tena na tena, bila kuiweka chini mpaka uielewe. Nafsi yako ni ya muhimu zaidi kuliko ulimwengu mzima. "Mtu atafaidiwa nini kama akiupata ulimwengu wote lakini akiupoteza nafsi yake?
Simama na ahadi za Mungu ambazo hazibadiliki. Baada ya kuokoka, kunayo mambo matatu ambayo unahitajika kufanyia mazoezi kila siku kwa ukuaji wa roho. Kwanza ni kuomba, ambapo ni wakati unongea naye Mungu. Ya pili ni kusoma Bibilia yako, ndiposa Mungu aweze kunena nawe. Na ya mwisho, gawiza imani yako kwa wengine, ndiposa uweze kuongea kuhusu Mungu. "Kwa hiyo usione haya kushuhudia kuhusu Bwana wetu, wala usione haya mimi niliyefungwa kwaajili yake bali ushiriki pamoja nami taabu ya injili kwa kadri ya nguvu ya Mungu. (2 Timotheo 1:8) "Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu mimi nami nitamkiri mbele za baba yangu aliye binguni. "(Mathayo 10:32) Unahitaji kubatizwa kwa kutii Mwokozi Yesu Kristo, kama ushuhuda kwa umma wa wokovu, na kasha uungane na kanisa ambayo inaamini Bibilia.